# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA FEDHA

Anwani ya simu: Hazina, Dodoma,
Simu: +255-26-2160000,
Nukushi : +255-26-2963109,
Barua pepe: ps©hazina.go.tz
Tovuti: www.mof.go.tz

Mji wa Serikali - Mtumba,
Mtaa wa Hazina,
S.L.P. 2802,
40468 DODOMA.

Unapojibu tafadhali taja:

**Kumb. Na. PST/GEN/2023/01/67**

**27 Julai 2023**

Maafisa Masuuli Wote,
**TANZANIA BARA.**

**WARAKA WA HAZINA NA. 2 WA MWAKA 2023/24 KUHUSU MATUMIZI YA MFUMO MPYA WA USIMAMIZI WA UNUNUZI WA UMMA KWA NJIA YA KIELEKTRONIKI *(NATIONAL e-PROCUREMENT SYSTEM OF TANZANIA - NeST)***

---

## 1. UTANGULIZI

Kila mwaka Serikali inatumia sehemu kubwa ya fedha zinazoidhinishwa kwenye bajeti za Mafungu mbalimbali kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa, kandarasi za ujenzi na huduma kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma, SURA 410 na Kanuni zake. Aidha, Serikali imeendelea kudhibiti matumizi ya fedha zinazopelekwa kwenye kila Fungu kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo mifumo ya kielektroniki ili kuleta tija na ufanisi unaostahili katika utekelezaji wa Bajeti ya Fungu husika. Kwa mujibu wa **Kifungu cha 9(1)(k) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410**, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imekasimiwa jukumu la kusanifu, kuanzisha na kuhuisha mifumo mbalimbali ya kielektroniki kwa ajili ya kuweka uwazi na kuleta tija kwenye ununuzi wa umma.

Katika kuhakikisha Taasisi Nunuzi zinatumia Mfumo wa Kielektroniki katika uendeshaji wa michakato yote ya ununuzi wa umma, mwaka 2019 Serikali ilianzisha Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma *(Tanzania National e-Procurement System – TANePS)* ambao ulikuwa ukisimamiwa na PPRA. Katika kuhimiza matumizi ya Mfumo huo, tarehe 23 Oktoba, 2019, kupitia **Waraka wa Hazina Na. 4 wa mwaka 2019**, nilitoa maelekezo kwa Taasisi Nunuzi zote kutumia Mfumo wa TANePS baada ya kubaini kuwa baadhi ya Taasisi Nunuzi zilikuwa zinaendesha michakato ya ununuzi wa umma nje ya Mfumo huo. Licha ya Mfumo huo kutumika, ilibainika kuwa na changamoto mbalimbali kwa Taasisi Nunuzi na wazabuni.

## 2. UJENZI WA MFUMO MPYA WA UNUNUZI WA UMMA

Ili kukabiliana na changamoto mbalimbali za matumizi ya Mfumo wa TANePS, mwezi Julai 2022, Serikali ilianza ujenzi wa Mfumo mpya wa Usimamizi wa Ununuzi wa

Umma wa Kielektroniki (National e-Procurement System of Tanzania – NeST), ambao ujenzi wake unasimamiwa na PPRA. Hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2023, ujenzi wa moduli mbili za NeST ulikuwa umekamilika. Moduli hizo ni: Moduli ya Usajili wa Watumiaji, Huduma na Bidhaa (e-Registration) na Moduli ya Kuendesha Mchakato wa Ununuzi (e-Tendering). Hizi ni kati ya Moduli sita zinazotarajiwa kujengwa katika Mfumo huu mpya. Ujenzi wa NeST unatarajiwa kukidhi mahitaji ya Nchi kwenye eneo la Ununuzi wa Umma na kukabiliana na changamoto za Mfumo wa Ununuzi unaotumika sasa (TANePS).

## 3. LENGO NA MADHUMUNI YA WARAKA

Lengo la Waraka huu ni kuwafahamisha Maafisa Masuuli wote kuhusu utumiaji wa Mfumo mpya wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST). Maafisa Masuuli wote mnaelekezwa kuhakikisha kuwa Taasisi Nunuzi zilizopo kwenye Mafungu yenu, zinatumia Mfumo huo katika ununuzi wote unaotumia fedha za umma. Utumiaji wa Mfumo wa NeST utasaidia katika kuongeza uwazi,ushindani na usawa katika shughuli za ununuzi, kupunguza mianya ya rushwa na kupata thamani halisi ya fedha katika Ununuzi wa Umma. Mfumo wa NeST unapatikana kwa kupitia anuani ya *https://www.nest.go.tz*.

## 4. MATUMIZI YA MFUMO MPYA WA UNUNUZI (NeST)

Maafisa Masuuli wote mnaelekezwa kuanza kutumia Mfumo mpya wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST) katika michakato yote ya ununuzi wa umma. PPRA inaelekezwa kuendelea kutoa mafunzo kwa Taasisi Nunuzi zote juu ya matumizi ya NeST ili kuhakikisha kuwa Taasisi Nunuzi zote zinatumia NeST ifikapo tarehe 30 Septemba, 2023. Aidha, Taasisi Nunuzi ambazo tayari zimepata mafunzo zinaelekezwa kuanza kutumia Mfumo huo kuanzia mwezi Julai 2023. Endapo kutakuwa na changamoto yoyote ya kiufundi au kiutaalam unaokwamisha matumizi ya Mfumo huo, Taasisi Nunuzi na Wadau wanatakiwa kuwasiliana na PPRA mapema iwezekanavyo kwa namba za simu ***+255-736-494-948*** pamoja na barua pepe ***support@nest.go.tz*** ili kuhakikisha mnapata ufumbuzi unaostahili. Inasisitizwa kwamba, **kuanzia tarehe 1 Oktoba 2023, Taasisi Nunuzi hazitoruhusiwa kufanya ununuzi wa umma nje ya Mfumo wa NeST.** Taasisi Nunuzi ambayo itafanya ununuzi wowote bila kutumia Mfumo wa NeST, itakuwa imetenda kosa na hivyo itachukuliwa hatua zinazostahili kwa mujibu wa Sheria.

## 5. MAFUNZO

Watumishi wa umma wote wanaohusika na mchakato wa ununuzi ndani ya Taasisi Nunuzi wanapaswa kupata mafunzo yatakayowawezesha kuutumia Mfumo wa NeST kwa ufasaha. Mafunzo ya matumizi ya Mfumo huu yanaendelea kutolewa na Mamlaka kwenye vituo vilivyopo kwenye Mikoa ifuatayo: Dodoma, Iringa, Dar es salaam, Mwanza, Arusha na Mbeya. Ratiba za mafunzo zinapatikana kwenye Mfumo wa usimamizi wa mafunzo na semina (*Training and Seminar Management System (TSMS))* unaopatikana kwenye anuani ya ***"tsms.ppra.go.tz"***. Watumiaji wa Mfumo wa NeST

wanaopaswa kushiriki mafunzo haya ni pamoja na Afisa Masuuli, Wakuu wa kitengo/Idara ya Ununuzi, Wakuu wote wa Idara, Maafisa wawili kwa kila idara wanaohusika na kuanzisha ununuzi wa idara, Mkaguzi wa Ndani, Maafisa Tehema na Mwanasheria wa Taasisi Nunuzi.

## 6. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

Maafisa Maasuuli wote mnapaswa kuzingatia yafuatayo:

(i) Wazabuni na wamiliki wa kampuni nchini wanaotarajia kufanya biashara na Serikali wanatakiwa kuhudhuria Mafunzo ya Mfumo wa NeST, kujisajili na kuingiza taarifa zinazohitajika kwa ajili ya kupata huduma mbalimbali zinazotolewa na Mfumo ikiwemo kuwasilisha zabuni kupitia Mfumo huo. Taasisi Nunuzi zinaelekezwa kuwajulisha Wazabuni watarajiwa kuhusu utumiaji wa Mfumo mpya wa NeST katika michakato yote ya Ununuzi wa Umma ili waweze kutumia Mfumo huo kwa ufanisi na kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu na Miongozo ya Ununuzi wa Umma iliyopo;

(ii) Ili kuanza kutumia Mfumo wa NeST, Taasisi Nunuzi zinatakiwa kuwasilisha PPRA majina mawili ya maafisa watakaokua wasimamizi wa Mfumo (System Administrators) kwa kupakua fomu inayopatikana kwenye anuani ***https://www.nest.go.tz/documents/forms.*** Fomu hii ijazwe na kusainiwa na Afisa Masuuli na kupigwa muhuri wa Taasisi. Msimamizi huyo atasajiliwa na PPRA na baada ya hapo atatakiwa kuwasajili na kusimamia watumiaji wengine wote walioko ndani ya taasisi.

(iii) Taasisi Nunuzi zitakazoendelea na ununuzi ndani ya Mfumo wa TANePS mpaka tarehe 30 Septemba, 2023 zinapaswa kutengeneza mpango wa Ununuzi wa mwaka (APP) na kuwasilisha kwenye Mfumo wa TANePS. Hata hivyo, Taasisi itakapopatiwa mafunzo ya Mfumo wa NeST haitaruhusiwa kuanzisha zabuni yoyote ndani ya Mfumo wa TANePS bali watatakiwa kuanza kutumia Mfumo wa NeST mara moja.

(iv) Ifikapo tarehe 1 Oktoba, 2023 Taasisi Nunuzi zote za Serikali hazitaweza kutuma mialiko ya zabuni kwenye Mfumo wa TANePS na badala yake zitapaswa kutumia Mfumo wa NeST. **Mfumo wa TANePS utafikia ukomo wa matumizi tarehe 30 Septemba 2023**. Baada ya tarehe hiyo Mfumo wa TANePS hautapatikana hewani kwa ajili ya matumizi ya Ununuzi wa Umma isipokuwa kwa shughuli za ndani kama kupata taarifa za ununuzi.

(v) Kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2023 mpaka tarehe 31, Desemba 2023, Mfumo wa TANePS hautapokea malipo ya ada za usajili mpya kwa wazabuni. Malipo yatakayopokelewa kwa kipindi hicho ni ada za kutangaza zabuni (Taasisi Nunuzi) na ada ya kuomba zabuni (Mzabuni). Zabuni zitakazoruhusiwa kutangazwa kwenye Mfumo wa TANePS kwa kipindi hicho

ni zabuni za muda mfupi tu pamoja na CUIS ambazo mchakato wake wa kupata mshindi utakuwa umekamilika pale ifikapo tarehe 31 Desemba, 2023. Aidha, PPRA itahakikisha kuwa wazabuni waliokwisha lipa fedha za usajili TANePS na muda wao haujamalizika, muda huo utahamishiwa kwenye Mfumo wa NeST.

(vi) Taasisi Nunuzi zinatakiwa kuhakikisha zinaandaa bajeti sahihi inayoakisi ununuzi halisi unaofanyika kwa kila idara ndani ya Taasisi hizo. Mfumo wa NeST utachukua moja kwa moja bajeti iliyoandaliwa kwenye mifumo ya kibajeti na kuitumia kwenye mchakato mzima wa ununuzi na kuandaa Mpango wa Ununuzi wa Mwaka (APP).

(vii) Wazabuni wanatakiwa kuhakikisha wanahuisha taarifa zao kwenye Mamlaka mbalimbali za usajili ikiwemo BRELA, CRB, ERB, AQRB, n.k, kuwa na leseni sahihi ya biashara na kuweka taarifa sahihi wakati wa kujisajili.

(viii) Watumiaji wa Mfumo wanatakiwa kupata msaada zaidi kuhusu Mfumo kwa kuwasiliana na **PPRA kwa namba za simu +255-736-494-948** pamoja na barua pepe ya support@nest.go.tz

**7. TAREHE YA KUTUMIKA KWA WARAKA**

Waraka utaanza kutumika kuanzia tarehe ya waraka huu na hivyo **unafuta Waraka Na. 4 wa Mwaka 2019 wenye Kumb. Na. EB/AG/485/01/Vol.XII/26 wa tarehe 23 Oktoba 2019.** Aidha, Taasisi Nunuzi zihakikishe zinahudhuria mafunzo yanayotolewa na Mamlaka na **kwamba Taasisi zote zitaanza kutumia Mfumo kuanzia 1 Oktoba, 2023**.

**8. HITIMISHO**

Serikali kupitia Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na PPRA inaendelea kuboresha mifumo wa ununuzi kwa lengo la kuongeza ufanisi na thamani ya fedha katika Ununuzi wa Umma. Katika kufikia azma hiyo, ni wajibu wa kila Afisa Masuuli kuzingatia maelekezo ya Waraka huu Pamoja na Sheria, Kanuni na Miongozo ya Ununuzi wa Umma. Pamoja na ratiba ya mafunzo, PPRA itatoa mwongozo wa matumizi ya Mfumo wa NeST.

Mwamba

Dkt. Natu E. Mwamba
**KATIBU MKUU NA**
**MLIPAJI MKUU WA SERIKALI**

**Nakala kwa**: Katibu Mkuu Kiongozi,
Ofisi ya Rais – IKULU,
1 Barabara ya Julius Nyerere,
CHAMWINO,
S.L.P. 1102,
**40400 DODOMA.**

Katibu Mkuu,
Ofisi ya Rais,
Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI),
Mji wa Serikali- Mtumba,
Mtaa wa TAMISEMI,
S.L.P. 1923,
**41185 DODOMA.**

Katibu Mkuu,
Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu),
2 Mtaa wa Reli,
S.L.P. 980,
**40480 DODOMA.**

Mwanasheria Mkuu wa Serikali,
Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,
Mji wa Serikali - Mtumba,
Mtaa wa Mwanasheria,
S.L.P. 630,
**DODOMA.**

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali,
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu,
4 Barabara ya Ukaguzi,
S.L.P. 950,
**41104 DODOMA.**

Msajili wa Hazina,
Ofisi ya Msajili wa Hazina,
Jengo la CHC,
50 Mtaa wa Mirambo/Samora,
S.L.P. 3193,
**11104 DAR ES SALAAM.**

Afisa Mtendaji Mkuu,
Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA),
Jengo la Kambarage, Ghorofa ya 9,
Barabara ya PSPF,
S. L. P 2865,
**41104 DODOMA.**